JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA ISHIRINI

KIKAO CHA KUMI NA NANE

28 JUNI 2010

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA ISHIRINI

KIKAO CHA KUMI NA NANE – TAREHE 28 JUNI, 2010

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii kwa Mwaka wa Fedha, 2010/2011.

MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII:

Taarifa ya Kamati ya Huduma za Jamii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010

pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha, 2010/2011.

MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII:

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

WAZIRI WA MIUNDOMBINU:

Randama za Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Miundombinu kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

II. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

121. MHESHIMIWA ESTHER KABADI NYAWAZWA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Hospitali ya Wilaya Geita licha ya

kuhudumia Kata (33) ina Madaktari Bingwa wawili (2) tu, na upanuzi wa hospitali unasuasua na utawala ni mbovu:-

Je, ni lini Serikali itarekebisha matatizo hayo.

122. MHESHIMIWA HAFIDH ALI TAHIR (DIMANI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Moja kati ya sababu zinazosababisha wanafunzi wengi kufeli katika mitihani yao ni ukosefu wa maabara mashuleni:-

(a) Je, ni asilimia ngapi ya shule za Serikali (za sekondari na msingi) zenye maabara na ngapi hazina maabara;

(b) Je, ni asilimia ngapi ya shule za seminari zina maabara na ngapi zisizo na maabara ambazo Serikali imezisaidia.

WIZARA YA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

123. MHESHIMIWA KAPT. JOHN DAMIANO KOMBA (MBINGA MAGHARIBI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia:- Kampuni ya simu ya **TIGO** ilijenga mnara wa mawasiliano kwenye Mji mdogo wa Lituhi tangu mwaka 2007 lakini hadi sasa haujaanza kutumika:-

(a) Je, mnara huo utaanza kutumika lini, na mawasiliano yanaweza kuwafikia wananchi wa maeneo ya Kata ya Ngumbo umbali wa kilometa 35;

(b) Je, ni nani atalipa gharama ikiwa uharibifu wowote utatokea hasa

ikizingatiwa kuwa hakuna mlinzi kwenye eneo hilo.

WIZARA YA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:

124. MHESHIMIWA GOSBERT BEGUMISA BLANDES (KARAGWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika:- Bei ya Kahawa inayolipwa Karagwe iko chini ikilinganishwa na ile inayolipwa nchi jirani ya Uganda:-

Je, ni kwa nini bei ya Kahawa inayolipwa kwa wakulima wa Uganda isilipwe pia kwa wakulima wa Karagwe.

125. MHESHIMIWA TATU MUSA NTIMIZI (IGALULA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika:- Mkoa wa Tabora ni moja kati ya Mikoa inayolima kwa wingi Tumbaku ya kukausha na ndilo zao kuu la kiuchumi kwa wananchi wa Tabora:-

(a) Je, Serikali itawasaidia vipi wakulima wa zao hilo, ikiwa wao hutumia kuni kukaushia Tumbaku na Serikali hukataza ukataji wa miti ovyo;

(b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwapatia wakulima hao Makaa ya Mawe kama njia mbadala ya kukaushia Tumbaku yao ili kuzuia ukataji miti ovyo na hivyo kuepusha Tabora kuwa jangwa.

WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:

126. MHESHIMIWA MARIA IBESHI HEWA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko:- Katika Mkutano wa Bajeti ya Mwaka 2008/2009 ilitolewa hoja ya kuteketezwa kwa Kiwanda cha Ngozi cha Ilemela na Waziri mhusika aliombwa kutembelea Kiwanda hicho:-

Je, Waziri alitimiza ombi hilo na anasema nini kuhusu kukifufua kiwanda hicho.

WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

127. MHESHIMIWA MICHAEL LEKULE LAIZER (LONGIDO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:- Wilaya ya Longido haina Hakimu wa Wilaya jambo linalowafanya wananchi wake kufuata huduma za Kimahakama kwenye Mahakama ya Wilaya ya Monduli umbali wa zaidi ya km. 160:-

(a) Je, ni lini Serikali itajenga Mahakama ya Wilaya;

(b) Je, Serikali ipo tayari kupeleka Hakimu wa Wilaya ili kupunguza

usumbufu wa kwenda Mahakama ya Monduli.

WIZARA YA MIUNDOMBINU:

128. MHESHIMIWA JACOB DALALI SHIBILITI (MISUNGWI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu:- Tanroads imekuwa ikiifanyia matengenezo mazuri barabara ya Misasi – Kasololo – Sumbugu – Mbarika lakini bado kuna maeneo ya Manawa Ginnery na sehemu za Sumbugu hadi Mbarika:-

Je, Serikali inasema nini juu ya kufanya matengenezo hayo kwa mwaka huu.

WIZARA YA NISHATI NA MADINI:

129. MHESHIMIWA HERBERT JAMES MNTANGI (MUHEZA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:- Maeneo yanayotolewa leseni za utafutaji wa Madini ni makubwa kiasi cha kuingia hata ndani ya maeneo ya wananchi, ya vijiji vilivyopimwa na mashamba yenye hati:-

Je, kwa nini taarifa za utoaji leseni za utafuataji wa madini kwenye maeneo ya kijiji kilichoandikishwa zisiwekwe bayana kwa kijiji kinachohusika.

130. MHESHIMIWA DUNSTAN DANIEL MKAPA (NANYUMBU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:- Umeme wa gesi wa Mnazi Bay Mkoani Mtwara sasa umeshafika Masasi:-

(a) Je, ni lini sasa umeme huo utafika Wilayani Nanyumbu;

(b) Je, kuna mipango mingine mbadala ya kuipatia umeme Wilaya ya Nanyumbu.

III. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:

Kwamba, Bunge likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa Mwaka wa Fedha, 2010/2011.

DODOMA **DKT. T.D. KASHILILAH**
28 JUNI, 2010 **KATIBU WA BUNGE**